

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MAGU**  
(Barua zote zipelekwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)

**MKOA WA MWANZA**

Simu:- 028 – 2530002

FaxNo.:-028 – 2530199



Sanduku la Posta 200  
**MAGU.**

Kumb.Na.MDC/S.10/69/81

12.09.2017

---

## **TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

1.0. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu anawatangazia wananchi wote wenye sifa zilizoainishwa hapa chini kutuma maombi ya kazi katika Halmashauri ya Magu kwa kazi ya Afisa Mtendaji wa Kijiji daraja III.

### **1.1 Mtendaji wa Kijiji - (Village Executive III) Nafasi 25**

#### **Sifa za kuajiriwa moja kwa moja: -**

- i) Awe na Elimu ya kidato cha nne na kuendelea.
- ii) Awe na Astashahada, cheti cha Utawala, Sheria Elimu ya Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo – Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.
- iii) Awe na akili timamu
- iv) Awe raia wa Tanzania
- v) Awe na umri wa miaka kati ya 18 – 45
- vi) Awe tayari kufanya kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Magu eneo lolote atakalopangiwa
- vii) Asiwe mwajiriwa katika Utumishi wa Umma au aliyewahi kuajiriwa na kufukuzwa katika katika Utumishi wa Umma,

#### **Majukumu: -**

- i) Atakuwa Mtendaji Mkuu wa Kijiji na mshauri wa Serikali ya Kijiji na Kamati zake katika mipango ya Maendeleo.
- ii) Atakuwa Katibu na Mtunza kumbukumbu za vikao vyote vya Kijiji.
- iii) Atakuwa Afisa Mhasibu wa Serikali ya Kijiji na atasimamia Mapato na Matumizi ya Serikali ya Kijiji.
- iv) Atakuwa kiongozi wa Watendaji wengine wa Kijiji.
- v) Atakuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala bora katika Kijiji.

- vi) Ataratibu na kusimamia utekelezaji wa Sheria ndogondogo za Serikali ya Kijiji.
- vii) Atasimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji.
- viii) Atafanya kazi nyingine kama atakavyoelekezwa na Mkuu wake wa kazi.

**Kiwango cha Mshahara:**

TGS B – Tshs 390,000/= kwa mwezi

**2.0. Masharti ya Jumla kwa waombaji:**

Waombaji wote wanatakiwa kuambatisha vitu vifuatavyo: -

- i) Barua ya maombi iliyoandaliwa kwa mkono
- ii) Picha 2 (mbili) ndogo za hivi karibuni
- iii) Wasifu wa mwombaji (CV)
- iv) Vyeti vya kuzaliwa, shule na Taaluma – Vithibitishwe na Hakimu ama Wakili – Results Slip na Progress Report hazitakubaliwa.
- v) Awe na Umri chini ya miaka 38
- vi) Asiwe amewahi kuhukumiwa kifungo jela au kufukuzwa kazi.
- vii) Mwombaji awe tayari kufanya kazi Magu pasipo kuhama ndani ya miaka mitatu.

**3.0. Usaili:**

Tarehe ya Usaili kwa waombaji watakaofanikiwa kufaulu kwenye mchujo **(Shortlisting)** itatangazwa. Aidha, siku ya Usaili mwombaji aje na vyeti halisi vya ELimu na Taaluma. Taarifa ya Polisi (Loss Report) kuhusiana na vyeti , Result slip havitapokelewa.

**4.0. Ajira:**

Mwombaji atakayefanikiwa atajulishwa tarehe ya kuripoti.


Tarehe ya mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 05/10/2017 saa 9.30 Mchana.

**Maombi yatumwe kwa:-**

Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya ya Magu,  
S.L.P 200

**MAGU.**

Imetolewa na: -



Lutengano G. Mwalwiba  
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**